Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara Kuhusu Nambari ya IMEI.pdf 1 06/09/2023 13:16

Kipeperushi hiki kimeandaliwa kama sehemu ya Mpango wa Elimu kwa Mtumiaji wa Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya (CA).




## 1. IMEI ni nini?

IMEI ni ufupisho wa *International Mobile Equipment Identity*, ambao ni Utambulisho wa Kimataifa wa Kifaa cha Simu. Hii ni nambari maalum iliyokabidhiwa kila kifaa cha simu ya GSM na kwa kawaida ina tarakimu 15 au 16.

## 2. Madhumuni ya nambari ya IMEI ni yapi?

Madhumuni ya kimsingi ya nambari ya IMEI ni kutambua vifaa vya simu. Jukumu jingine ni kuzuia wizi. Ikiwa kifaa cha simu kinaweza kutambuliwa kimataifa, mwizi hawezi kubadilisha kadi ya SIM kwenye simu na atarajie kwamba atakaa na simu hiyo. Kwa hivyo, itasaidia sana endapo kifaa cha simu kitaibwa kupiga ripoti kwa asasi za kutekeleza sheria pamoja na kwa mtoa huduma wa simu za mkononi.

Ni muhimu sana kuthibitisha ikiwa kifaa cha simu ni halali au ghushi.

## 3. Je, vifaa vyote vya simu ya rununu vina nambari za IMEI?

La, baadhi ya vifaa vya simu havina nambari za IMEI. Hii ni kwa sababu mara nyingi vifaa hivyo ni ghushi na kwa hivyo, Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya (CA) haijaziidhinisha kutumika nchini.

## 4. Je, nitajua vipi nambari ya IMEI ya kifaa changu?

Kwenye baadhi ya vifaa vya simu ya mkononi, nambari ya IMEI imechapishwa ndani ya sehemu ya betri. Hata hivyo, mtu pia anaweza kuulizia nambari ya IMEI ya kifaa chake cha simu ya mkononi kwa kubofya *#06# kwenye kidayo, au pamoja na maelezo mengine ya mfumo katika menyu ya mipangilio kwenye mifumo ya uendeshaji ya simu. Katika hali nyingi, mtu hawezi kunakili na kubandika nambari hiyo, kwa hivyo mtu anahitaji kuiandika pembeni ili kuihifadhi vyema.

## 5. Je, kifaa cha simu kilicho na kadi mbili za SIM kina IMEI ngapi?

Vifaa vya simu vinavyoweza kubeba zaidi ya kadi moja ya SIM vina zaidi ya IMEI moja. Kutokana na hilo, kifaa cha simu chenye SIM mbili kina nambari mbili za kipekee za IMEI.

## 6. Mtu anawezaje kuthibitisha nambari ya IMEI ya kifaa cha simu?

Mtu anaweza kuthibitisha nambari ya IMEI ya kifaa cha simu ya kwa kutuma nambari ya IMEI kwa nambari fupi ya 1555.

## 7. Huduma ya Uthibitishaji wa IMEI ya 1555 ni nini?

Hii ni huduma ya upigaji simu bila malipo inayotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano ili kuwapa Wakenya fursa ya kuthibitisha nambari za IMEI za vifaa vya simu.

## 8. Ninafaa kufanya nini endapo jibu la huduma ya 1555 linaonyesha maelezo ya kifaa cha simu yaliyo tofauti na ya kifaa changu cha simu?

Ripoti visa vyote vya simu ghushi kwa Mamlaka kwa kutumia anwani zilizotolewa kwenye kipeperushi hiki.

## 9. Ninaweza kuthibitisha nambari yangu ya IMEI kupitia 1555 mara ngapi kwa siku?

Unaweza kuthibitisha mara mbili (2) pekee kwa siku.

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara Kuhusu Nambari ya IMEI.pdf 2 06/09/2023 13:16

## Unahitaji kufahamu zaidi?

Kwa habari zaidi kuhusu mada iliyopo hapo juu au sehemu nyingine yoyote ya afya na usalama wa mitambo ya mawasiliano, tafadhali wasiliana na:

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA

*OPENING YOUR WORLD*

**Head Office**
CA Centre, Waiyaki Way, P.O. Box 14448, Nairobi 00800
Mobile: 0703042000, Email: complaints@ca.go.ke
Complaints: chukuahatua@ca.go.ke
020-445 5555, 0714 455 555, 0737 455 555

**CA Western Regional Office**
1st Floor KVDA Plaza
P.O. Box 2346
Eldoret 30100
Mobile: 0703042105
Email: wro@ca.go.ke

**CA Coast Regional Office**
3rd Floor, NSSF Building
P.O. Box 8041
Mombasa 80100
Mobile: 0703042152
Email: cro@ca.go.ke

**Central Regional Office**
Ground Floor, Advocates Plaza
P.O Box 134
Nyeri 10100
Mobile : 0703042181
Email : cero@ca.go.ke

**Nyanza Regional Office**
2nd Floor Lake Basin Mall,
P.O Box 2016
Kisumu 40100
Mobile: 0703042130
Email: nro@ca.go.ke

Communications Authority of Kenya
@ca_kenya

**Ilani ya kujitoa hatarini:** Huku kila jaribio likiwa limefanywa ili kuhakikisha kuwa habari iliyojumuishwa katika hati hii ni sahihi, imekusudiwa TU kuwa kama mwongozo wa kuelekeza utendakazi salama wa mitambo ya mawasiliano na haipaswi kuchukuliwa kama (au kutumika badala ya) ushauri wa kisheria. Kwa hivyo, Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya haitakubali kosa lolote kwa matokeo ya hatua zozote zilizochukuliwa, au maamuzi yaliyotolewa kwa misingi ya taarifa iliyotolewa.

**CA/PEA/CEP/KIS/F/4/2021**

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA

www.ca.go.ke

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara Kuhusu Nambari ya IMEI

